

Mwongozo wa Shughuli Za Kampeni Ya Mwaka Wa 2026

Utangulizi:

Katika mwaka wa 2026, kwa pamoja tunaungana kwa ajili ya kampeni ya Siku 16 za Uanaharakati chini ya dhamira ya "**Tengeneza Upya Mamlaka Yetu: Hatua za pamoja Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake"** na kauli mbiu "*Wezesha, Chukua Hatua, Tengeneza Mustakabali wa Baadae.*"

Tunaadhimisha kampeni ya mwaka huu wakati ambapo mashirika mengi yanayo tetea haki za wanawake, wanaharakati, na vuguvugu za uanaharakati zinapitia kipindi ambacho nafasi ya kiraia inaminywa, kutokuwepo na utulivu wa kisiasa, uwanda wa mtandaoni wenye sumu,, taarifa potofu, simulizi zenye kupinga haki za binadamu na kupungua kwa rasilimali. Changamoto hizi zinatufanya tuone umuhimu zaidi wa kuimarisha mamlaka yetu kwa pamoja na kutafuta njia za kuendeleza kazi ya kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake.

Kiti ya Kuchukua Hatua na utetezi ya mwaka 2026 inajumuisha nyenzo za usaidizi wa shughuli za kampeni: utepe wa zambarau; Bango la A3; sumaku za jokofu; kadi za uthibitisho; kalenda ya dawati ya mwaka 2027; pedi za kipanya; mifuko ya kubebea vitu; na nyaraka za kampeni ikijumuisha: Muhtasari wa Kampeni; Mwongozo wa Shughuli za Kampeni; Mwongozo wa Kampeni za Vyombo vya Habari

Nyenzo hizi za shughuli zinaweza kubadilishwa kulingana na muktadha na kutumika katika ngazi za **mtu binafsi, shirika, na jamii**, kulingana na muktadha wako, hadhira, vipaumbele, na uwezo.

Mwaka huu, tunakualika utumie Siku hizi 16 sio tu kuongeza uelewa, bali pia kutafakari, kujiunganisha, kujiandaa, kutetea, na kuchukua hatua kwa pamoja. Jiunge nasi na **Wezesha, Chukua Hatua, Tengeneza Mustakabali wa Baadae**

16 DAYS

GBV PREVENTION NETWORK

UN TRUST FUND TO END VIOLENCE AGAINST WOMEN AND GIRLS

1. Fahamu vizuri kuhusu Kiti ya Kampeni



- Kiti ya Kuchukua hatua na utetezi ina nyenzo muhimu za kukusaidia ili uweze kushiriki katika kampeni ya Siku 16. ***Muhtasari wa Kampeni*** unatoa maelezo yafuatayo: usuli, mantiki, malengo, na jumbe muhimu za kampeni ya mwaka wa 2026. **Mwongozo wa Shughuli za Kampeni** unatoa shughuli zinazopendekezwa kwa watu binafsi, mashirika, na jamii.
- **Mwongozo wa Shughuli za Vyombo vya Habari** unatoa maelezo juu ya mawazo na vitendea kazi kwaajili ya kuwasilisha kampeni kupitia mitandao ya kijamii na majukwaa mengine ya vyombo vya habari.
- Nyenzo zingine zilizomo kwenye kiti, ni pamoja na **bango, utepe wa zambarau na mweupe, kadi za uthibitisho, sumaku za jokofu, kalenda za mwaka wa 2027, pedi za kipanya, na mifuko ya kubebea vitu;** vinaweza kutumika kwa njia ya ubunifu ili kuchangamsha na kuwezesha mazungumzo, tafakari, utetezi na kuchukua hatua kwa pamoja.

Kabla ya kuanza shughuli za kampeni yako, tenga muda wa kuzifahamu vyema nyenzo zilizomo na kutafakari maana ya "*Kutengeneza Upya Mamlaka Yetu*" katika muktadha wako. Zingatia mamlaka ya pamoja ambayo tayari ipo ndani ya shirika lako, jamii, au vuguvugu lako, changamoto zinazoweza kuleta vikwazo katika kuchukua hatua za pamoja, na washirika na wadau watarajiwa wanaoweza kuimarisha jitihada zenu. Tafakari mambo mnayoweza kufanikisha kwa pamoja ambayo yasingewezekana mkiwa peke yenu, na bainisha hatua madhubuti mnazoweza kuchukua katika kipindi cha Siku 16 zitakazosaidia kujenga kasi na kuzidi kuendelea hata baada ya kampeni kukamilika.

2. Andaa Majadiliano ya Bango la Kampeni

Bango la kampeni linaangazia dhamira kuu ya kampeni. Tumia bango kuandaa majadiliano; lengo ni kuchangamsha na kuongoza mazungumzo ya mtu mmoja mmoja au vikundi, majadiliano ambayo yanaweza kuchukua muda wa dakika 20 hadi 30, kutafakari jinsi mnavyoweza kutengeneza upya mamlaka zenu na za mtu binafsi au za pamoja na kuzielekeza katika kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

3. Jiunge kwenye mshikamano kwa Kuvaa Utepe

Sambaza na uvae utepe mweupe au wa rangi ya zambarau wenye ujumbe ***"Zuia Ukatili Dhidi ya Wanawake"*** kama ishara ya wazi ya mamlaka ya pamoja na dhamira ya kuzuia ukatili dhidi ya wanawake. Vaa utepe ili kufanya kampeni ionekane kwa njia ya uwazi. Zivae katika kipindi chote cha Siku 16, au wakati wa shughuli muhimu kama vile majadiliano ya kijamii, maandamano, shughuli kwenye sehemu za kazi na shuleni, pamoja na matukio yanayo fanyika hadharani. Wahimize watu wengine wajiunge kwa kuvaa utepe na kila mmoja kuchukua hatua ya kuwezesha, kuchukua hatua, au tengeneza mustakabali wa baadae

4. Sambaza Pedi za Kipanya cha Kompyuta (Mouse Pads) ili Kuchochea Tafakari

Sambaza na utumie pedi za kipanya cha kompyuta kama kitu cha ukumbusho unaoonekana kila siku kwa ajili ya kutafakari. Zinaweza kutumika ofisini, darasani, katika maeneo ya jamii na mazingira mengine yanayofaa ili kuchochea tafakari na mazungumzo kuhusu *"Kutengeneza Upya Mamlaka Yetu: Hatua za pamoja Kuzuia Ukatili Dhidi ya Wanawake"* Tumia ujumbe huo kutoa wito kwa watu kutafakari kuhusu mamlaka ya pamoja walionayo, kubaini kile wanachoweza kufanya kwa pamoja ili kupinga kanuni potofu zitokanazo na mila, na kuahidi hatua moja watakayochukua kwa vitendo ili kuzuia ukatili dhidi ya wanawake katika kipindi cha Siku 16 na kuendelea.

5. Peleka Ujumbe Kwa Kupitia Mifuko ya Kubebea Vitu (Tote Bags)

Tuma mifuko ya kubebea vitu kwenye ujumbe wa simu kwa ajili ya hatua za pamoja. Wahimize washiriki kubeba na kushirikisha mifuko ya kubebea vitu kazini, shuleni, sokoni, kwenye matukio ya kijamii, na maeneo ya umma, ili kufanya ujumbe uonekane katika maeneo yanayo tumika kila siku. Acha mifuko ianzishe mazungumzo kuhusu mamlaka ya pamoja, mshikamano, na kuchukua hatua kwa vitendo, geuza kitu kilichozoeleka kila siku na badala yake kitumike kuwakumbusha kila mmoja wetu kwamba ana jukumu la kufanya; na kwa pamoja, tunaweza kuleta mabadiliko ya kudumu.

6. Tumia Mwongozo wa Shughuli za Vyombo vya Habari ili Kuimarisha Hatua za Pamoja

Tumia Mwongozo wa Shughuli za Vyombo vya Habari ili kuimarisha hatua za pamoja na kushirikisha hadhira mbalimbali katika Siku 16. Mwongozo huu unatoa jumbe na mawazo yaliyo tayari kutumika kwenye mitandao ya Facebook, Instagram, BlueSky, WhatsApp, na majukwaa mengine, pamoja na vidokezo vya kiutendaji vya kufanya kazi na vyombo vya habari vya ndani. Badilisha maudhui haya kulingana na muktadha wako, shirikisha hadithi za hatua za pamoja, angazia sauti za watu na suluhisho, na tumia vyombo vya habari kuwawezesha, kuchukua hatua, na kutengeneza mustakabali wa baadae kuelekea kwenye dunia isiyo na Ukatili Dhidi ya Wanawake.

7. Buni Shughuli Zinazokidhi Mahitaji Mahususi

Rekebisha shughuli za Siku 16 kulingana na muktadha wako, vipaumbele, na hadhira. Tumia kiti hii kutengeneza nafasi ya kutafakari, kujiunganisha, kuchukua hatua za pamoja, na utetezi. Chagua shughuli zinazoweza kuwasaidia watu kutengeneza mamlaka yao, kuimarisha juhudi za pamoja, na kuchukua hatua zilizo madhubuti ili kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

Unapochagua shughuli, anza kwa kuzingatia hadhira unayolenga kuifikia, mabadiliko unayotarajia kuleta, na rasilimali ulizonazo. Chagua idadi chache ya hatua zinazoweza kutekelezeka, zenye umuhimu, na zinazohusiana na lengo kuu la kutengeneza mamlaka ya pamoja ya kuzuia ukatili dhidi ya wanawake.

Tunawatakia kampeni yenye mafanikio! Na tunatarajia kusikia kutoka kwenu kuhusu ushiriki wenu katika kampeni hii.

Timu ya Kuzuia Ukatili wa Kijinsia (UWAKI)